# THE MWALIMU NYERERE FOUNDATION

**HOTUBA YA**

**MHESHIMIWA DKT. SALIM AHMED SALIM,**
**MWENYEKITI WA TAASISI YA MWALIMU NYERERE**

**ALIYOITOA KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA**

Kijiji cha Boko,
Wilaya ya Kinondoni,
**DAR ES SALAAM**

16 Juni 2003

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SALIM AHMED SALIM, MWENYEKITI WA TAASISI YA MWALIMU NYERERE ALIYOITOA KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MTOTO WA AFRIKA, KIJIJI CHA BOKO WILAYA YA KINONDONI, DAR ES SALAAM TAREHE 16 JUNI, 2003.**

**Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto;**

**Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan; Waziri wa Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake na Watoto, Zanzibar;**

**Waheshimiwa Mawaziri na Naibu Mawaziri;**

**Luteni Yusuf Makamba; Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;**

**Makatibu Wakuu;**

**Mstahiki Kleist Sykes; Meya wa Jiji la Dar es Salaam,**

**Waheshimiwa Mabalozi na Wawakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Mashirika mbali mbali ya Kimataifa;**

**Viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa;**

**Viongozi wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali na Taasisi za Dini;**

**Watoto wapendwa;**

**Ndugu Wananchi;**

**Mabibi na Mabwana.**

Awali ya yote napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mheshimiwa Dkt. Asha-Rose Migiro (Mb), Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto kwa kunialika kuwa Mgeni Rasmi katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika, 2003.

Kwa namna ya pekee napenda kuwapongeza wananchi wote wa Mkoa wa Dar es Salaam na Mkuu wetu wa Mkoa huu Luteni Yusuf Makamba, kwa kukubali kuandaa maadhimisho haya kitaifa. Nakupongezeni pia wananchi wa kijiji cha Boko kwa mapokezi na maandalizi mazuri ambayo sote tumeyashuhudia.

**Ndugu Wananchi,**

Leo hii tupo hapa kijijini Boko kuadhimisha Siku ya Mtoto wa Afrika. Kwa hakika, siku hii ni muhimu sana katika bara letu la Afrika. Masuala yanayohusu maendeleo ya watoto yamepewa umuhimu wa hali ya juu katika nchi za Afrika na pia katika ngazi mbalimbali za kimataifa. Mtakumbuka, tarehe 16 Juni, 1976, katika Kitongoji cha Soweto, Afrika ya Kusini, mamia ya watoto wa shule waliandamana mtaani kupinga ubaguzi wa rangi na elimu

duni waliyokuwa wakipewa. Walidai haki yao ya kupewa elimu bora na sawa pamoja na kufundishwa katika lugha yao. Watoto 2,000 waliuwawa na maelfu waliumizwa na maaskari wa makaburu. Kwa kumbukumbu ya watoto hao waliouawa kutokana na ujasiri wao wa kuandamana wakidai haki yao, **Siku ya Mtoto wa Afrika** iliwekwa kuadhimishwa kila tarehe 16 Juni tangu mwaka 1991. Siku hii inatukumbusha maisha ya watoto wa Afrika, inatukumbusha pia kitendo cha watoto hao kutambua maovu yaliyokuwepo ndani ya utawala wa makaburu na kuandamana kupiga vita ubaguzi wa rangi. Aidha, kitendo hiki kinadhihirisha ufahamu wa hali ya juu walio nao watoto kuhusu masuala mbalimbali ya kutetea haki zao.

Kimataifa, msukumo mkubwa wa kuheshimu haki ya mtoto ulianza katika miaka ya themanini ambapo mwaka 1989, Mkataba wa Kimataifa wa Haki za mtoto ulipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa. Mwaka 1990 Wakuu wa Nchi mbalimbali duniani walikutana kwenye Makao Makuu ya Umoja wa Mataifa, New York, na kuweka mkakati wa kuendeleza masuala yanayohusu watoto. Jitihada hizi ni kielelezo cha namna ambavyo masuala ya watoto

yanapewa umuhimu katika ngazi ya juu kabisa ya jumuiya ya kimataifa.

Kwa upande wa bara letu la Afrika, Umoja wa Nchi Huru za Afrika (OAU), kupitia vikao vyake mbalimbali, mwaka 1990 ulipitisha Mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa Mtoto. Mkataba huu wa Afrika umemwangalia mtoto kwa mtazamo wa mazingira ya kiafrika.

Mimi binafsi nilipata bahati kushiriki na kuchangia kikamilifu katika matukio yote mawili haya ya kihstoria – yaani maamuzi ya Umoja wa Mataifa na Umoja wa Nchi Huru za Afrika. Nakumbuka fika changamoto na matumaini yaliyojengeka kutokana nayo.

**Ndugu Wananchi,**

Nchi yetu ya Tanzania imepiga hatua katika masuala ya kumwendeleza mtoto. Serikali ilipitisha Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya mwaka 1996 kwa Tanzania Bara na Sera ya Uhai, Hifadhi na Maendeleo ya Watoto ya mwaka 2000 kwa Zanzibar. Sera zote

hizi zinaainisha maeneo mbalimbali yaliyo muhimu kwa malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto wa Tanzania.

Hivyo basi, tunapoadhimisha siku ya Mtoto wa Afrika, tunatumia siku ya tarehe 16 Juni ya kila mwaka kutathmini na kutafakari utekelezaji wa mikataba ya kimataifa, sera na mikakati ambayo tumejiwekea kuhusu maendeleo na ustawi wa watoto.

**Ndugu Wananchi;**

Jitihada zote hizi za kitaifa na za kimataifa zitafanikiwa tu endapo tutajiuliza na tutathmini michango tunayoitoa katika kufanikisha utekelezaji wa sera, mikakati na mipango ambayo imewekwa kumwendeleza mtoto na kulinda haki zake ndani ya jamii katika taifa letu na bara la Afrika.

Mara nyingi kumekuwepo na fikra kwamba masuala ya kuwapatia haki na ustawi watoto ni wajibu wa Serikali, taasisi zisizo za kiserikali na mashirika ya dini. Katika siku hii ya leo, ni vema tukatafakari upya fikra hizi. Kwanza kabisa ipo haja ya kutambua kwamba jukumu la awali la malezi na makuzi ya mtoto

ni la baba na mama. Kimsingi, jukumu hili linaanzia toka mtoto akiwa bado tumboni mwa mama yake hadi kuzaliwa na hatimaye kufikia umri wa kuwa mtu mzima. Jambo lililo wazi ni kwamba sehemu kubwa ya matatizo yanayowakabili watoto hivi leo inatokana na sisi kama wazazi, familia au jamii kukwepa wajibu wa asili wa kulea kiumbe tunachokileta duniani.

**Ndugu Wananchi**, tunapoadhimisha Siku hii muhimu sana katika bara letu, ni vema tukaangalia upya mtazamo tulionao kuhusu majukumu yetu katika malezi na makuzi ya watoto. Matatizo yanayowakabili watoto wetu katika bara la Afrika ni makubwa.

Matatizo haya ya watoto yanaweza kugawanywa katika makundi makubwa manne.

**Kwanza** ni kundi la Watoto wa Mitaani (Street Children). Kundi hili linajumuisha mamilioni ya watoto waliozaliwa mitaani na kuishi mitaani pasipo kazi, makazi, wala kuwa na uhakika wa mlo wao wa siku. Kundi hili limejitokeza kuongezeka mijini kutokana na mvuto wa watoto kutoka vijijini kuja mijini. Matokeo yake ni

kusambaratika kwa watoto wetu hawa, kuongezeka kwa uhalifu pamoja na baadhi yao kujiingiza katika utumiaji au/na usambazaji wa madawa ya kulevya na taathira zake. Mchanganyiko wa hayo yote ni kubomoa mustakabali wowote ule mwema kwa jamii hii.

**Pili** ni kundi la Watoto wanaoajiriwa kwenye vikundi vya Majeshi ya upiganaji. Katika nchi nyingi za Afrika hususan, Liberia, Sierra Leone, Somalia, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Sudan na kadhalika watoto walio chini ya miaka 14 huingizwa ama kwa hiari lakini zaidi kwa njia za hadaa na vitisho kwenye makundi ya kijeshi na kufundishwa matumizi ya silaha wakiwa wadogo. Hali hii ni ukiukwaji wa haki za watoto na inaleta athari kubwa za kisaikolojia kwa makuzi na malezi ya watoto hao.

Kundi la **tatu** ni la Watoto wanaoingizwa au wanaojiingiza kwenye biashara ya ukahaba na umalaya. Kundi hili limejitokeza kuongezeka kwa kasi mijini na linatisha. Wengi wao ni watoto wa kike na wachache wa kiume wenye umri chini ya miaka 14. Madhara yake kiafya tunayajua wote, hususan watoto hawa wengi hujikuta wanaambukizwa Ukimwi na magonjwa mengine ya zinaa. Mwisho wake ni taifa kupoteza watoto wake na nguvu kazi yake.

Kundi la **nne** ni la watoto wadogo chini ya miaka 14 wanaoajiriwa ama kwa hiari yao au kwa nguvu na vitisho katika migodi; uvuvi; uuzaji wa madawa ya kulevya na kadhalika pasipo mishahara ya kukidhi mahitaji yao. Mbali ya Tanzania, nchi nyingi za Afrika zimekumbwa na tatizo hili, hususan Afrika ya Kusini, Zambia, Zimbabwe, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo na kadhalika. Takwimu zilizotolewa na Waziri Mkuu Frederick Sumaye hivi karibuni, zinaonyesha kuwepo na watoto 1.4 milioni katika kundi hili. Serikali imeweka lengo la kuondokana na ajira haramu ya watoto ifikapo mwaka 2010. Lengo hili ni zuri na linahitaji mshikamano kati ya jamii na Serikali. Ninashauri utekelezaji wake uharakishwe na ikiwezekana, lengo lifikiwe mapema kabla ya mwaka 2010 ili Taifa letu lisijikute limetumbukia katika janga la kuongezeka kwa ajira haramu ya watoto wadogo.

**Ndugu Wananchi;**

Katika mtazamo wa jumla, inadhihirika wazi kuwa makundi yote hayo yamekosa haki yao ya kuishi ambayo Jamii ingewapa na kuyasimamia.

Tukiacha familia, kwa maana ya baba na mama, lipo pia jukumu la jamii. Na hapa ningependa tuangalie jamii katika sura mbili. Sura ya kwanza ni "familia", yaani ndugu wa karibu wa wazazi wa mtoto ambao hutoa miongozo na ushauri kwa baba na mama wa mtoto lakini hawana lile jukumu la awali la malezi. Hata hivyo, pale inapotokea kifo cha mmoja wa wazazi au wote wawili, basi hawa huweza kubeba jukumu la kumlea mtoto ambaye wazazi wake wamepatwa na tatizo hilo. Kundi hili hujumuisha watu kama shangazi, wajomba, babu, bibi, na ndugu wengine.

Sura ya pili ni ya jamii. Sura hii inahusu watu wanaoishi karibu na wazazi wa mtoto. Jamii hii huwa na wajibu wa jumla wa malezi na makuzi ya mtoto hata kama hawana uhusiano wa damu na mtoto huyo. Jukumu hili katika mazingira ya nchi zetu za kiafrika hutokana hasa na mila nzuri na desturi, na mfumo wa kijamii tuliojiwekea. Hivyo si jambo la ajabu kumkuta mtu mzima akimkemea au akimuasa mtoto wa jirani yake au hata wa mtu asiyemfahamu.

Lakini jukumu la majirani haliishii hapa tu. Wakati mwingine majirani au wakazi wa sehemu fulani wanaweza wakatoa msaada endapo mtoto amekabiliwa na matatizo maalum au hata wakatoa hifadhi. Katika siku za hivi karibuni tumeshuhudia matukio ambapo jirani tu wameweza kutoa taarifa za ukatili kwa watoto, au hata kuchukua hatua za kuvijulisha vyombo vya dola. Haya yote yanaonyesha kwamba kwa hakika ukiacha baba na mama, ndugu wa wazazi, jirani na jamii kwa ujumla wana mchango wa aina fulani katika malezi, makuzi na maendeleo ya mtoto.

**Ndugu Wananchi,**

Tukiyatazama haya yote tutaona kwamba, tuna ulazima wa kuchukulia siku ya leo kama fursa ya kutazama upya tunayatekeleza vipi majukumu yetu, ya kumlea, kumkuza na kumuendeleza mtoto. Ni nafasi nzuri ya kutafakari upya jinsi majukumu yetu kama wazazi, kama familia na kama jamii yanavyoendana na azma ya Serikali katika sera mbalimbali za kulinda haki za watoto.

**Ndugu Wananchi,**

Nisingependa siku ya leo kuzungumzia sana nini majukumu ya Serikali au Serikali inafanya nini katika kuhamasisha au hata kushinikiza maendeleo ya mtoto. Itoshe tu kusema kwamba Serikali imepitisha sera na kuweka mazingira mazuri ya kutekeleza sera hizo, imepitisha sheria mbalimbali, yote hayo kwa lengo la kuwezesha jamii kutimiza wajibu wake. Pamoja na sera zinazohusu maendeleo ya mtoto, Serikali kwa ushirikiano na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa muda mrefu wamekuwa wakitekeleza programu ya Uhai, Ulinzi na Maendeleo ya Mtoto Tanzania Bara na Zanzibar.

Programu hii imeleta mafanikio makubwa katika kumuendeleza mtoto. Baada ya jitihada hizi za Serikali na washirika wake, kazi kubwa inayotukabili ni kuongeza kasi kama wazazi, kama sehemu ya familia na kama jamii kwa ujumla wake, ya kuwalea watoto wetu kwa namna ambayo itawaletea maendeleo na ustawi.

**Ndugu Wananchi,**

Kwa kuzingatia umuhimu wa nafasi ya kila mmoja wetu kwa makuzi ya watoto, kaulimbiu ya mwaka huu ambayo inasema ***"Malezi Bora Utotoni, ni Msingi wa Maisha"*** imekuja wakati muafaka. Itakumbukwa kwamba katika miaka ya nyuma suala la malezi lilitazamwa kwa kusisitiza unyonyeshaji na kukamilisha chanjo. Mambo mengine yaliyofuata yalizingatia afya na elimu bora kwa ujumla wake. Hata hivyo, kutokana na matatizo mengi yanayowakabili watoto hivi sasa, imejitokeza haja ya kuipa sura mpya dhana ya malezi bora. Wataalam wanatueleza kwamba ili mtoto aweze kukua vizuri matunzo yake ni sharti yaanze toka akiwa tumboni kwa mama. Matunzo yake katika kipindi cha uja uzito wa mama yana uhusiano mkubwa na afya yake ya kimwili na kiakili atakapozaliwa. Ni kwa msingi huo **Ndugu Wananchi** tunasema kaulimbiu hii ***"Malezi Bora Utotoni, ni Msingi wa Maisha"*** imekuja wakati muafaka sana. Kwa upande wa bara la Afrika malezi bora katika hatua za mwanzo kabisa za maisha ya mtoto ni moja ya masuala muhimu yaliyopewa kipaumbele katika mkataba wa Afrika kuhusu Haki na Ustawi wa mtoto ambao Tanzania imeuridhia. Aidha, mkutano wa Afrika kuhusu watoto uliofanyika Cairo, Misri tarehe 28 hadi 31 Mei, 2001, ulizitaka Serikali zetu kuchukua hatua za kuhakikisha kuwa kila mtoto

barani Afrika anapata mwanzo mzuri katika maisha na anakuwa, kulelewa na kuendelezwa katika mazingira mazuri yenye upendo, amani, usalama na heshima ikiwa ni pamoja na kuthamini na kulinda haki za mtoto.

**Ndugu Wananchi**, kaulimbiu hii ya "***Malezi Bora Utotoni, ni Msingi wa Maisha***" ina umuhimu wa pekee katika kututia hamasa ya kutekeleza majukumu yetu mbalimbali katika kutoa malezi bora, hasa katika ngazi ya awali ya makuzi ya mtoto. Kama nilivyoeleza hapo awali, kwamba kuna uhusiano mkubwa kati ya matunzo bora ya awali na hali bora ya kiafya na ya kimwili ya mtoto hapo baadaye, hali kadhalika kuna uhusiano mkubwa kati ya makuzi ya watoto na ujenzi wa taifa bora la baadaye. Hivyo, Watoto hawa ni raslimali muhimu katika uhai wa taifa letu na Afrika kwa ujumla. Wakati umefika kwetu sote kama jamii kuhakikisha kwamba tunalipa kipaumbele suala la malezi bora utotoni ili tuweze kujenga msingi imara wa maisha kwa watoto wetu na hatimaye taifa zima. Tukiazimia leo hii na kuweka nguvu zetu pamoja, sina shaka tutafanikiwa kuwajengea watoto wetu mazingira mazuri ambayo yataleta hali bora zaidi ya maisha yao.

**Ndugu Wananchi,**

Maadhimisho haya yamepambwa na shughuli mbalimbali nchini kote na Afrika kwa ujumla. Ninafahamu vema kwamba ili kufanikisha shughuli hizi misaada na michango ya watu mbalimbali imetumika. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru UNICEF, Care International, Jetha Dilips, Top Screen and Craft, Kunduchi Water Parks Limited, taasisi mbalimbali, makampuni na watu binafsi ambao kwa namna moja au nyingine wanashirikiana na Serikali katika kuwaendeleza watoto hapa nchini na wameshiriki pia katika kufanikisha maadhimisho haya.

Nisingependa hata kidogo kusahau risala nzuri ya watoto ambayo kwetu sisi sote tulio hapa ni changamoto na ya kufanyiwa kazi. Aidha, niwapongeze wale wote waliotunukiwa zawadi. Sina shaka jamii yetu kwa ujumla itaendelea kuwatia hamasa na kuwaenzi watoto wetu wote ambao kama tulivyoona wameonyesha jitihada kubwa katika nyanja na maeneo mbalimbali. Ni matumaini yangu pia kuwa kama jamii tutayatazama matatizo ya watoto, tutayatatua ili kusimamia haki ya mtoto wa Afrika tutafanikiwa kumjengea misingi mizuri ya

maendeleo mtoto wa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Haki ya kuishi kwa mtoto wa Afrika ni changamoto kwetu. Daima tuidumishe na tujiulize tutaitekelezaje? Ni jukumu letu sote. Tukiwaondolea adha watoto wetu tutafanikiwa kuiondolea kero jamii yetu.

**Ndugu Wananchi,**

Ni matumaini yangu kuwa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika kitakuwa mwanzo wa kujenga upya misingi ya kijamii itakayotupa fursa ya kutoa malezi bora ya watoto wetu kuanzia tumboni mwa mama, utotoni, hadi kufikia umri wa kujitegemea kwani malezi hayo ndiyo msingi wa maisha endelevu ya taifa letu.

**Nakutakieni nyote maadhimisho mema.**

**Ahsanteni kwa kunisikiliza.**